KISWAHILI: KARATASI YA 1

Maagizo

a) Karatasi hii ina sehemu tano kuu

b) Jibu maswali yote kulingana na maagizo

Soma mazungumzo yafuatauo kisha ujibu maswali yanayofuata.

(Ni nyumbani kwa Kubai, babuye Kaima. Kaima amemtembelea babuye kijijini baada ya kufunga shule, siku ya Jumamosi. Kaima ni mwanafunzi wa Gredi ya 7. Begani amebeba mkoba wenye kipakatalishi. Mkononi ameshika rununu. Babu anamwona kwa mbali ila hamtambui kwa urahisi.)

Babu: (Akijisemea.) Vitoto vya siku hizi vinakua upesi mno. Utadhani vimetiliwa mbolea. Ama tuseme vimepandwa kwenye udongo wenye rutuba. Lakini mbolea gani? Hii tu niliyotilia mtama wangu na haukumea hata chembe! Labda mvua iliyonyesha haikutosha. Au tuseme ni tatizo la tabianchi. Sijui mimi ... (Kaima anakaribia aliko Babu. Babu anamtambua na kumwita kwa sauti.) Mjukuu wangu! Mjukuu wangu! (Kwa furaha.)

Kaima: Naam! (Akimkaribia.) Shikamoo babu!

Babu: (Huku akimkumbatia.) ____1. mjukuu wangu. Umefanya vyema kuja kunijiulia hali. Hakika nilikuona kwa mbali nikashindwa kukutambua kwa haraka. Habari za shule?

Kaima: Njema babu. Tulifunga juzi. Tuko likizoni. Nilikuwa na hamu kubwa ya kuja kukutembelea.

Babu: Nashukuru sana kwa uamuzi wako. Hakika umekuwa mkubwa.

Kaima: (Huku akitabasamu.) Asante Babu. Shibe ya pale skuli inatunenepesha kweli. (Akicheka.)

Babu: (Akimwashiria kiti akae.) Nilikwambia mwanamume ni nguvuze. Vinginevyo utakuwa ng'onda.

Kaima: (Wakicheka.) Pokea salamu za mamangu. Wanapanga kuja kukutembelea hivi karibuni. Anamsubiri dadangu atoke ughaibuni juma lijalo.

Babu: (Akitabasamu.) Nafurahi sana kusikia kwamba nyote mko salama mjini. Nina hamu kubwa kuwapokea. (Babu anamkaribisha kwa chajio. Wanaonekana kukifurahia kwa pamoja.)

1. Babu angetumia neno gani katika nafasi yenye nambari 1?
   A. Sijambo
   B. Marahaba
   C. Sina la kuamba
   D. Aheri

2. Kwa mujibu wa mazungumzo haya;
   A. mtama wa babu haukumea kutokana na ubovu wa mbolea.
   B. mtama wa babu haukumea kwa kuwa mvua haikutosha.
   C. mtama wa babu haukumea kwa kuwa haukuwa mzuri.
   D. haijulikani kwa nini mtama wa babu haukumea.

3. Unadhani kwa nini babu hakumtambua mjukuu wake kwa haraka?
   A. Mjukuu alikuwa amewekewa mbolea
   B. Mjukuu alikuwa amebeba kipakatalishi na simu
   C. Mjukuu alikuwa amekua sana
   D. Mjukuu alikuwa amekaa sana bila kumtembelea

4. Babu anaposema kuwa 'utakuwa ng'onda', ametumia fani gani ya lugha?
   A. Tashbihi
   B. Sitiari
   C. Tanakali
   D. ashihisi